## 03. MAHITAJI YA SHULE KWA WANAFUNZI WOTE WA BWENI NA KUTWA:-

Mwanafunzi anatakiwa afike na mahitaji yafuatayo siku ya kuripoti shuleni

- 3.1. Rimu 1 ya karatasi kwa mwaka kwa ajili ya kufanyia majaribio na mitihani.
- 3.2. Faili (spring file) dogo kwa ajili ya kutunza kumbukumbu za mwanafunzi
- 3.3. Michango ya chakula /uji isipokuwa kwa wanafunzi wenye mahitaaji maalum.
    - Mahindi kg60 kwa mwaka kwa mwanafunzi wa kutwa na kg 120 kwa mwanafunzi wa bweni
    - Maharage kg30 kwa mwaka kwa mwanafunzi wa kutwa na kg60 kwa mwanafunzi wa bweni
    - Mchele kg10 kwa wanafunzi wa kutwa na kg20 kwa wanafunzi wa bweni
    - Sukari kg07 kwa wanafunzi wa kutwa na kg08 kwa wanafunzi wa bweni
    - Gharama za uendeshaji Tsh 60,000 kwa mwaka kwa mwanafunzi wa kutwa na Tsh 220, 000 kwa mwaka kwa mwanafunzi wa bweni

        - Michango hii inaweza kulipwa kwa awamu mbili mpaka tatu yaani Januari, Aprili na Julai.

**MUHIMU:** Mpango wa shule ni kuhakikisha wanafunzzi wote wanapata chakula cha mcchana shuleni.

### 3.3 SARE YA SHULE

**WAVULANA**

- Suruali mbili zisizobana rangi ya kijani jeshi zenye urefu wa kufunika visigino pasipo kuzikanyaga. zenye upana wa ichi 21- 22 miguuni
- Shati mbili nyeupe za mikono mifupi aina ya tetroni zenye mfuko mmoja upande wa kushoto zisizobana.
- Mkanda mweusi upana usiozidi inchi 2
- Jozi ya viatu rangi nyeusi vya ngozi vya kufunga kwa kamba vyenye visigino vifupi.
- Soksi nyeusi jozi 2.

**WASICHANA**

- Sketi mbili rangi ya kijani jeshi zenye marinda ya kuelekea upande mmoja. Upana wa marinda inchi 2. upana wa mkanda usiozidi inchi 2. Sketi iwe na urefu wa kutosha ya heshima. Wanafunzi wenye sketi fupi hawatapokelewa.
- Shati mbili nyeupe za mikono mifupi aina ya tetroni zenye mfuko mmoja upande wa kushoto zisizobana. Kwa wanafunzi wa kiislam wawe na Panjabi yenye mikono mirefu na jarabibi nyeupe.
- Jozi ya viatu rangi nyeusi vya ngozi vya kufunga kwa kamba vyenye visigino vifupi.
- Soksi nyeupe jozi 2.

